



## BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA

### TAREHE YA MITIHANI YA LESENI KWA WATAHINIWA WANAORUDIA MITIHANI YA LESENI NA WATARAJALI (POST INTERN)

Ofisi ya Msajili - Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010 Sehemu ya II Kipengele cha 6 (a) inapenda kuwajulisha kuwa mitihani ya leseni itafanyika tarehe 06/11/2020 siku ya Ijumaa kuanzia saa tatu kamili asubuhi.

Mitihani hii itafanyika kwa watahiniwa ambao wanarudia mitihani na watarajali (post intern) ambao wanamaliza mafunzo ya vitendo mwishoni mwa mwezi Oktoba, 2020. Hivyo, watahiniwa wanapaswa kukamilisha taratibu zifuatazo:-

1. Kujaza fomu ya maombi na kuambatanisha vyeti vyote vya taaluma, vyeti vya sekondari pamoja na picha nne za rangi (Four coloured passport size)
2. Kukamilisha malipo ya mtihani wa leseni na usajili. Malipo ya mtihani huu ni shilingi **150,000/=** kwa wale wanaofanya kwa mara ya kwanza na shilingi **75,000/=** kwa wale wanaorudia. Mwisho wa malipo hayo ni tarehe 15/10/2020, kinyume chake mhusika atalipia kwa nyongeza kama ilivyoainishwa katika mwongozo wa mitihani ya leseni kwa Wauguzi na Wakunga nchini
3. Malipo yote yatafanyika kwa kutumia mfumo wa malipo ya serikali (GePG) Hivyo watahiniwa watapaswa kuwasiliana na ofisi ya Msajili kwa ajili ya kupata kumbukumbu namba ya malipo (control number). Malipo yanaweza kufanyika kwa mmoja mmoja au kwa kikundi ikiambatishwa na orodha ya majina ya walipaji. Mwombaji ambaye hatakamilisha malipo ya mtihani huu hataruhusiwa kufanya mtihani
4. Mtahiniwa anatakiwa kuchagua kituo cha mtihani kati ya vituo vilivyoorodheshwa hapa chini. Vituo hivi havitabadilishwa ili kuepuka usumbufu

5. Kuwasilisha maombi ya kufanya mihani wa leseni na usajili Ofisi ya Msajili, Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania kabla ya tarehe 15/10/2020 kwa anuani ifuatayo;

Msajili – Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania  
Jengo la PSSF, Dodoma Plaza  
Ghorofa ya 5  
Barabara ya Benjamin Mkapa  
S.L.P 1736  
**DODOMA**

**Simu Na. 0737962691, 262966062/3- TNMC -Dodoma**

  
Msajili

**Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania**  
**31/08/2020**

**1. Jedwali linaloonyesha orodha ya vituo vya mitihani**

SN	Kituo	Mkoa
1	Tandabui- Taasisi ya Afya	Mwanza
2	Lugalo Chuo cha Uuguzi na Ukunga	Dar es Salaam
3	St. John –Dodoma -Chuo cha Uuguzi na Ukunga	Dodoma
4	KCMC Chuo cha Uuguzi na Ukunga	Kilimanjaro
5	PHCI-Iringa	Iringa
6	Mbeya – OTM	Mbeya
7	Mtwara Chuo cha Uuguzi na Ukunga	Mtwara
8	Morogoro Center of Distance Learning – kwa waliosoma njia ya Masafa kituo cha Morogoro	Morogoro